TOLEO LA. 04

# Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | SEPTEMBA 2020



## SHINYANGA YASIMAMA NA MAGUFULI

Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**

# TAHARIRI

## TAUSIKUBALI HOJA MUFISILI YA ACT WAZALENDO KUHUSU GESI

Wakati kampeni za kuwania Urais, Ubunge na Udiwani zikiendelea nchini, leo Chama cha ACT Wazalendo kimeendeleza utamaduni wake wa kupotosha kila juhudi zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo kimsingi inasaidia kuleta maendeleo ya watu.

Leo katika uzinduzi rasmi wa Chama hicho ulifanyika Lindi Mjini na kukosa mvuto huku kukiwa na mwitikio mdogo wa wananchi, amesikika Kiongozi Mkuu wa Chama, Zitto Kabwe amejaribu kuwahadaa wananchi wachache waliohudhuriauzinduzi huo kwa kusema kuwa gesi inayopatikana haijawanufaisha wananchi wa Kanda ya Kusini na watanzania kwa ujumla.

Tunapenda kumkumbusha Zitto kuwa Gesi imekuwa na manufaa makubwa ambapo gesi inayopatikana imewezesha kuzalisha umeme katika mitambo ya Kinyerezi I, Kinyerezi I-Extension na Kinyerezi II ambapo hadi kufikia Disemba mwakahuu,jumla ya megawati 583.22 zitakuwa zimeingizwa katika gridi ya Taifa ambazo zinatumika nchi nzima ikiwemo mikoa ya Lindi na Mtwara.

Tunawafahamisha tu Zitto na ACT Wazalendo kwamba gesi asilia kwa sasa imeunganishwa katika kiwanda cha Saruji cha Dangote ambacho kimetoa ajira lukuki kwa wananchi wa Lindi na Mtwara na watanzania kwa ujumla na pia kuongeza upatikanaji wa saruji nchini.

Mpaka sas TPDC imesambaza gesi asilia kwa nyumba zaidi ya 500 na viwanda 48 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Pwani, magari zaidi ya 400 yanatumia gesi asilia. Hii ni faida nyingine ambayo ACT Wazalendo hawaiona walakuonesha uzalando.

Serikali ikekamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambaji gesi (trunk lines) yenye urefu wa kilometa 17 na uwezo wa kuunganisha wateja zaidi 3000 wa majumbani katika mkoa wa Mtwara, kilometa 18 zenye uwezo wa kuunganisha wateja zaidi ya 10,000 katika mkoa wa Dar es Salaam na kilometa sita zenye uwezo wa kuunganisha
zaidi ya viwanda 20 katika mkoa wa Pwani.

Kwa upande wa mradi wa Gesi ya Liquefied NaturalGas (LNG) unaotarajiwa kutekelezwa katika eneo la Likong'o, mkoani Lindi, Serikali imelipa fidia zaidi ya shilingi bilioni tano ili kupisha mradi ambao utawezesha kusafirisha na kuuza gesi nje ya nchi na fedha zinazopatikana zinatumika kuwaletea wananchi maendeleo.

Tunapenda kuwakumbusha na kuwasisitiza wananchi kuwa makini na wanasiasa wachumiatumbo ambao ajenda yao kubwa ni kupotosha, kutukana na kuwahadaa wapiga kura badala ya kuuza Sera. Tutambue kwamba Urais sio mahali pa kufanyia majaribio. Uongozi unahitaji mtu makini, mkweli na mchapa kazi.

# DKT. MAGUFULI ASHUSHA NEEMA SHINYANGA

Na Mwandishi Wetu **- SHINYANGA**

Mgombea Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amesema katika miaka mitano ijayo Mkoa wa Shinyanga utashushiwa 'neema' kutokana na miradi mikubwa itakayotekelezwa kwenye mkoa huo na hivyo kuwaletea maendeleo zaidi zikiwemo ajira.

Rais Magufuli amesema hayo leo wakati wa mkutano wake wa hadhara kuomba kura kwa wananchi wa mkoa huo mjini Shinyanga katika uwanja vya Kambarage ili pate ridhaa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

"Mkituchagua tena pamoja na miradi mikubwa tutakayotekeleza, tutakuwa na jukumu la kujenga viwanda vya kuchakata nyama na kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kujenga na kuimarisha viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo ili tuzalishe ajira nyingi zaidi," alieleza Rais Dkt. Magufuli.

Ameeleza kuwa Serikali ya CCM Kwa upande wa miundombinu ya barabara amesema kuwa jumla ya kilomita 5,974 za barabara nchini zimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tayari kwa ujenzi kwa kiwango cha lami zikiwemo za mkoa wa Shinyanga ambazo mbali na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa na mazao pia zitazalisha ajira kwa wananchi wa mkoa huo.

Amesema Serikali itaongeza uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo kama maziwa kutoka bilioni 2.7 hadi lita bilioni 4.5, nyama nyekundu kutoka tani 690,629 hadi tani 790,000 na kuku kutoka tani 82,500 hadi tani 150,000. Ongezeko hilo la uzalishaji litaongeza ajira na kukuza kipato kwa wananchi.

Ameeleza kuwa machinjio mbili za kisasa zimejengwa katika mkoa huo ikiwemo yenye uwezo wa kuchinja mifugo 500 kwa siku na nyingine mifugo 100 kwa siku na zimekuwa na manufaa makubwa kwa watu wa Shinyanga.

Akizungumzia miradi ya maji iliyotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano Rais Dkt. Magufuli amesema imegharimu bilioni 60.8 na imewanufaisha wakazi wa Maganzo, Msalala, Kishapu, Mwadui, Muhunze na maeneo mengine ya mkoa huo.

"Katika kukuza uzalishaji wa nishati tumekamilisha mradi mkubwa wa kusafirisha umeme kutoka Iringa, Dodoma hadi Shinyanga na tutakapokamilisha mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere umeme utakuwa wa kutosha katika maeneo yote," amesisitiza Dkt. Magufuli.

"Ujenzi wa reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa (SGR) utagharimu zaidi ya trilioni tatu kwa kipande cha Mwanza hadi Isaka na utazalisha ajira nyingi na kuchochea ukuaji wa uchumi," alieleza Rais Magufuli.

# SHINYANGA WATAKA RAIS MCHAPAKAZI ANAYEMCHA MUNGU

Na Mwandishi Wetu - **SHINYANGA**

Wananchi wa Shinyanga pamoja na Viongozi wa Dini wa mkoa huo, wamemuomba Mwenyezi Mungu kuwaongoza watanzania kumchagua Rais wa aina ya Magufuli ambaye atakuwa ni Mchapakazi na anayemcha Mungu ili alete maendeleo ya kweli kwa watanzania.

Maombi hayo yamefanyika leo katika Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga muda mfupi kabla Mgombea Urais kwa tiketi uya Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli hajaongea na umati wa wananchi waliofurika uwanjani kumsikiliza.

Wamesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Tanzania inahitaji sana Kiongozi ambaye atafanya kazi kwa bidii kubwa ya kuwatumikia wananchi huku akimtanguliza Mungu katika kila jambo ili nchi ipate maendeleo lakini pia iwe na amani na utulivu.

"Watanzania na Mataifa yameshuhudia jinsi ambavyo Kiongozi wetu alivyokuwa mnyenyekevu mbele ya Mwenyezi Mungu na tuna uhakika katika miaka mitano utamsimamisha tena kwa ajili ya kuliongoza Taifa hili," alisikika Askofu Raphael Machimu, akimumuomba Mungu aipatie Tanzania Rais wa aina ya Magufuli katika uchaguzi Mkuu wa Octoba 28, 2020.

Akiendelea na maombi hayo Askofu Machimu amemuelezea Rais Magufuli kama Kiongozi aliyeleta maendeleo makubwa pasipo kumsahau Mungu na hata janga la Covid-19 bado aliwashirikisha Viongozi wa dini na wananchi kuliombea Taifa dhidi ya ugonjwa huo.

Kwa upande wake Sheikh wa Mkoa wa Shinyanga, Ismail Habib dua kwa Mwenyezi Mungu kama kuna mgombea anahamasisha uvunjivu wa amani, upendo, kuvunja undugu na asiyelitakia mema Taifa, basi asipate uongozi kwani ataliangamiza Taifa.

# KIKWETE: WATANZANIA MCHAGUENI MAGUFULI

- **Asema Kazi Kubwa Imefanyika Kukuza Uchumi**
- **Mitano Tena Kazi Iendelee**

Na Mwandishi Wetu - **CHALINZE**

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti Mstaafu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mhe. Jakaya Kikwete, amesema katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu Tano chini ya uongozi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, yamefanyika mambo mengi ambayo watanzania wanapaswa kupongeza na kumchagua tena Magufuli kwa miaka mingine mitano.

"Katika kipindi cha miaka mitano hii mmefanya kazi kubwa, kazi nzuri ya kukuza uchumi wa viwanda, kukuza ajira, kuimarisha huduma za jamii. Tunaona uchumi unaendelea kukua, tumepiga hatua kubwa kama nchi sioni sababu ya watanzania kutomchagua Magufuli lazima tufanye uamuzi sahihi," alisema Kikwete.

Kikwete ameyasema hayo leo Septemba 3, 2020 katika Mji Mdogo wa Chalinze mkoani Pwani wakati wa mkutano wa Kampeni wa Mgombea Mwenza nafasi ya Urais ambaye ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Akifafanua amesema kuwa Serikali zote zinazosimamiwa na CCM zimekuwa zikihakikisha maendeleo yanapatikana na hivyo hakuna sababu ya kuchagua vyama vingine.

"Katika kipindi changu nilifanya mengi, na kipindi hiki pia tunaona mengi yanafanyika, kwa hiyo kwenye nafasi ya Urais kura zote kwa Magufuli, na pia Wabunge na Madiwani kura zote kwa CCM," alisisitiza Rais Mstaafu Kikwete huku akishangiliwa na watu waliohudhuria mkutano huo.

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alisema katika kipindi kijacho watahakikisha maendeleo zaidi yanapatikana.

"Nawaomba sana wakazi wa Chalinze, tuchagueni tena, mchagueni Dkt. John Pombe Magufuli ili nasi tumsaidie kuleta maendeleo," aliwambo kura wananchi wa Chalinze.

Kwa upande wake mgombea ubunge Jimbo la Chalinze Ridhiwani Kikwete alisema kuwaSerikali ilitenga zaidi ya bilioni 17.1 Kwa ajili ya usambazaji wa maji safi na salama ambapo wakazi wa Chalinze wanapata maji hayo kwa uhakika kupitia vioski na kumwomba Mheshimiwa Samia kushughulikia suala la kuwaletea maji jirani na maeneo wanayoishi.

# MFUKO WA BARABARA KUIMARISHWA NDANI YA MIAKA MITANO

Na Mwandishi Wetu - **CHALINZE**

Serikali itaendelea kuimarisha mfuko wa barabara ili uweze kuwa na mgawanyo mzuri wa fedha kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) hatua ambayo inalenga kuimarisha ujenzi na ukarabati wa barabara hizo.

Kauli hiyo imetolewa na mgombea mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni  Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia mkutano wa Kampeni katika wa Rais wa Jamhuri  ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia mkutano wa Kampeni katika uwanja wa Miembe Saba Kata ya Bwilingu katika Mji Mdogo wa Chalinze, mkoa wa Pwani.

"Serikali itahakikisha inaimarisha mfuko Alisema katika hatua zote hizo za ujenzi, Serikali ya CCM itahakikisha wananchi wanalipwa fidia zao kwa wakati.

wa barabara ili kuwe na mgawanyo mzuri kati ya TANROAD na TARURA ili ziweze kujenga na kukarabati barabara zetu hizi kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi cha kwanza tumejenga na endapo mtatuchagua tutaendelea kuzikenga," ameeleza Mama Samia.

Akifafanua amesema kuwa TANROAD na TARURA zinafanya kazi nzuri lakini ipo haja yakuimarisha mfuko wa ujenzi wa barabara ili kuzipa nguvu na nafasi ya kusimamia ujenzi kwa wakati.

Kwa upande wake mgombea ubunge jimbo la Chalinze kupitia CCM, Ridhiwani Kikwete ameeleleza changamoto ya miundombinu ya barabara hususan zile za vijijini ambapo Mhe. Samia amemhakikishia kuwa mipango ya sasa ni kuboresha barabara zote nchini zikiwepo za Jimbo la Chalinze.

Amettaja baadhi ya barabara zitakazojengwa katika miaka mitano ijayo katika mkoa wa Pwani ni ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara zilizopo katika mkoa wa Pwani ikiwepo inayoanzia Makurunge kuelekea Saadani, Pangani hadi Tanga yenye kilomita 178, barabara ya Kisarawe-Maneromango yenye urefu wa kilomita 44, ujenzi wa Barabara ya Kibaha- Chalinze kwa njia nane na ujenzi wa daraja jipya la kisasa la Wami.

Alisema katika hatua zote hizo za ujenzi, Serikali ya CCM itahakikisha wananchi wanalipwa fidia zao kwa wakati.

Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia mkutano wa Kampeni katika uwanja wa Miembe Saba Kata ya Bwilingu katika Mji Mdogo wa Chalinze, mkoa wa Pwani.

"Serikali itahakikisha inaimarisha mfuko wa barabara ili kuwe na mgawanyo mzuri kati ya TANROAD na TARURA ili ziweze kujenga na kukarabati barabara zetu hizi kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi cha kwanza tumejenga na endapo mtatuchagua tutaendelea kuzikenga," ameeleza Mama Samia.

Akifafanua amesema kuwa TANROAD na TARURA zinafanya kazi nzuri lakini ipo haja yakuimarisha mfuko wa ujenzi wa barabara ili kuzipa nguvu na nafasi ya kusimamia ujenzi kwa wakati.

# LONGIDO HAITAKI MCHEZO 2020

**• Yaanza na Madiwani 18 Kupita Bila Kupingwa**
**• Safari ya Kumpa 100% Magufuli, Kiluswa Yaanza Rasmi**

Na Mwandishi Wetu **- Longido, Arusha**

Utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli umewafanya wananchi wa Longido mkoani Arusha kuwasahau kabisa wapinzani baada ya kufanikisha wagombea 18 wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa Udiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido kupita bila kupingwa.

Hatua hiyo ya kuiunga mkono CCM imetokana na Serikali kutekeleza ahadi zake kwa kishindo ikiwemo upatikanaji wa maji safi na salama kama anavyotanabaisha Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa aliyefika Uwanja wa Polisi-Longido kumuombea kura Dkt. Magufuli pamoja na Mgombea Ubunge wa Jimbo la Longido, Dkt. Stephen Kiluswa. Mhe. Majaliwa anaeleza namna Serikali ya Awamu ya Tano ilivyowajali

wananchi wa Longido kwa kuwaondolea adha ya muda mrefu ya ukosefu wa maji.

"Jambo kubwa lililokuwa linasumbua Longido ni upatikanaji wa maji safi na salama, Serikali iliamua kutoa shilingi bilioni 15.8 kwa ajili ya mradi wa majisafi mji wa Longido ambao utahudumia mji wa longido na vitongoji vyake. Mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na wananchi wanapata maji."

Mhe. Majaliwa anaongeza kuwa mbali ya mradi huo mkubwa wa kutoa maji kutoka Mto Simba mkoani Kilimanjaro hadi Longido, pia Serikali imetoa shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majisafi katika mji wa Namanga wilayani Longido na usanifu wa mradi huo umekamilika na kwamba wananchi wa Mji huo uliopo mpakani mwa Tanznia na Kenya watarajie neema ya maji katika Awamu ya Pili ya uongozi wa Rais Magufuli. Amesema lengo la Serik-ali ya CCMkutekeleza miradi hiyo ni kuhakikisha kila kijiji nchini kinakuwa na maji ya kutosha. "Maji lazima yatoshe na ndio sababu ya Serikali ilianzisha kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani na kazi hiyo Rais Magufuli ameifanya. Kutokana na juhudi hizo za Serikali kuwaondolea changamoto, Mhe. Majaliwa amewaomba wananchi wa wilaya ya Longido na Tanzania kwa ujuma wahakikishe wanampigia kura za kutosha Rais Dkt. John Pombe Magufuli na wagombea wake wote katika ngazi ya Ubunge na Udiwani nchini.

Pia Mhe. Majaliwa amewapongeza wananchi wa Wilaya ya Longido kwa kutambua mchango mkubwa wa maendeleo uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuwapitisha wagombea udiwani wa CCM katika kata zote 18 za wilaya hiyo bila ya kupingwa na kuwataka sasa Madiwani hao kuzunguka vitongoji vyote vya Wilaya hiyo kumuombea kura Rais Magufuli pamoja na Dkt. Kiluswa katika nafasi ya Ubunge.

# WANA-SHINYANGA NILETEENI PATROBAS KATAMBI BUNGENI - RAIS MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu - **SHINYANGA**

Mgombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM) nafasi ya Urais na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli amewaomba wananchi wa Jimbo la Shinyanga kumchagua Bw. Patrobas Katambi kuwa mbunge kwa sababu ni mchapa kazi hodari.

"Naomba Shinyanga mniletee huyu kijana (Patrobas Katambi) Bungeni, ni kijana mchapa kazi, ninampenda na ana historia nzuri na Shinyanga na anaipenda Shinyanga. Ni kijana ninayemuamini.

Katambi ni kijana mchapa kazi na ameamua kuacha nafasi ya ukuu wa Wilaya, tena Makao Makuu ya nchi kuja kuwatumikia wananchi wa Shinyanga hivyo nawaomba tena nichagulieni huyu kijana pamoja na Wabunge wote na Madiwani wa CCM ili tuendeleze kazi tuliyoianza ya kuwaletea maendeleo," alisisitiza Rais Magufuli.

Kwa upande wake, Patrobas Katambi ambaye anagombea Ubunge Jimbo Shinyanga Mjini kwa tiketi ya CCM, amesema Chama hicho kimewatendea wananchi wa Shinyanga mambo makubwa na kuwataka kuwapuuza wale wanaopita kwa kutumia lugha tamu kuwahadaa wapiga kura kwa ahadi zisizotekelezeka.

Alitaja baadhi ya miradi iliyotekelezwa na thamani yake kuwa ni pamoja na Elimu bilioni 6.7, Afya bilioni 2.1, Miundombinu 25.1, Kilimo na Mifugo bilioni 4.3, Mikopo kwa Vijana, wanawake na walemavu bilioni 8.61.

# MAGUFULI AFANANISHWA NA NABII MUSA

Na Mwandishi Wetu - **SHINYANGA**

Utendaji kazi uliotukuka wa Rais Magufuli katika kipindi cha miaka mitano tangu aingie madarakani umewafanya viongozi mbalimba kumfananisha na Nabii Musa alivyowatoa Wairael katika utumwa na mateso nchini Misri.

Mgombea Ubunge Jimbo la Shinyanga Mjini kupitia CCM, Patrobas Katambi amesema kuwa Rais Magufuli amekuwa kama Nabii Musa kutokana na kutekeleza ahadi na miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa wa Shinyanga.

Baadhi ya miradi iliyotekeleza Shinyanga ni elimuabure ambapo shilingi bilioni 6.7 zimetumika kuboresha elimu, shilingi bilioni 2.1 katika ujenzi wa hospitali za Wilaya na vituo vya afya, shilingi bilioni 25.1 katika miundombinu, shilingi bilioni 4.3 katika kilimo na mifugo pamoja na shilingi bilioni 8.61 kwa ajili ya mikopo kwa wakina mama na vijana pamoja na kuwathamini wachimabji wa wadogo wa madini.

Katambi ambaye anawafaha mu vizuri Viongozi wa CHADEMA na ACT Wazalendo, amewatahadharisha wananchi wa Shinyanga kutowapigia kura wagombea wa vyama hivyo kwa kuwa vyama hivyo vimepoteza mwelekeo na haviaminiki kwa kila vinachoahidi.

"Mheshimiwa Rais hawa wapinzani sio saizi yako, ninawafahamu vizuri, uwezo wao ni mdogo sana," ameeleza Katambi huku akishangiliwa na umati wa maelfu ya watu ambapo alitumia pia fursa hiyo kuwatahadharisha wapiga kura dhidi ya wanasiasa ambao Sera yao kubwa ni kupinga maendeleo yaliyoletwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mwaka 2015 Patrobas Katambi aligombea jimbo la Shinyanga Mjini kwa tiketi ya CHADEMA lakini baadae alikihama Chama hicho kutokana na Chama hicho kupoteza dira na mwelekeo na kugeuka Chama kinachopinga kila jambo jema linalotekelezawa na Serikali kwa manufaa ya wananchi.

Katika mkutano huo, Rais Magufuli amewaomba wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini kumchagua Patrobas Katambi kwani ni mchapakazi hodari na tayari amempa jukumu la kutatua kero zilizotolewa na wananchi katika mkutano huo.

# Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**